

KUFUWAWA KWA MIIKO YA SANAAJADIIYA KATIKA LUGHA ZA KIAFRIKA

Joachim A. N. Kisanji na Yusta Mganga

Joachim_kisanji@yahoo.com na mgangay@mstcdc.or.tz

Ikisiri

Makala hii inajadili kipera cha Miiko katika sanaajadiiya ya Lugha za Kiafrika. Miiko ni kipera kimojawapo cha sanaajadiiya ambacho kimesahaulika na wasomi hali inayosababisha Kufuwawa kwa miiko yenyewe katika matumizi ya kuiadilisha jamii. Matokeo ya kufuwawa huko ni kupotoka kwa maadili ya jamii. Kama zilivyo methali, nahau na vitendawili, miiko ina umuhimu wa kufunza maadili ya jamii na kuleta utengamano miongoni mwa jamii za Kiafrika. Nadharia ya kila jamii ina ujumi wake, fasihi ina kwao, na Ubuntu zinaweza kutumika katika kudhihirisha ni kwa jinsi gani miiko ni kipera adhimu kufundishwa na kutumika katika jamii ili kuibua tafakari ya elimu ya asili na kubainisha mapisi ya jamii za Waafrika katika nyanja mbalimbali za maisha hasa falsafa ya malezi na maadili. Hivyo, makala hii inanuia kujadili miiko katika ngazi ya maadili na malezi ambayo ndiyo msingi wa elimu ya utu kwa Waafrika. Kupotoka kwa maadili kunakosababishwa na kutabii usasa ni tatizo kubwa la malezi. Inatazamiwa kwamba makala hii itawanufaisha wataalamu wa Kiswahili, wakuza mitaala na mamlaka za elimu ya asili, hasa vipera vya sanaajadiiya kama miiko ili kutatua matatizo ya kupotoka kwa maadili katika jamii.